OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

# WIKI HII KWENYE MAGAZETI NA MITANDAO

02/09/2024 ► 06/09/2024

OAG

oagtanzania

www.oag.go.tz



*MINISTER of State in the President's Office (Public Service Management and Good Governance), George Simbachawene (centre) in conversation with the Minister of State in the Prime Minister's Office (Policy, Parliament and Coordination) William Lukuvi and Attorney General Hamza Johari in the National Assembly in Dodoma, yesterday. (Photo by Fadhili Akida)*

2 DAILY NEWS WEDNESDAY, SEPTEMBER 4, 2024

## From the National Assembly

From LYDIA SHEKIGHENDA and NELLY MTEMA in Dodoma

# Unauthorised deep-sea fishing attracts 2.7bn/- fine

THE government has introduced a new penalty for engaging in deep-sea fishing without a valid license or authorisation.

Under the updated regulations, individuals or entities caught fishing in deep-sea without proper permission could face fine of up to 1 million US dollars (about 2.7bn/-).

These changes are part of amendments to the Deep-Sea Fisheries Management and Development Act (Cap. 388), presented to the National Assembly through the Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill 2024. The bill, introduced by Attorney General Hamza Johari, was passed by lawmakers during its second and third readings on Monday.

In addition to the Deep-Sea Fisheries Management and Development Act, the bill amended the Mining Act (Cap. 123) and the Tanzania Fisheries Research Institute Act (Cap. 280).

The new provisions in the Deep-Sea Fisheries Management and Development Act aimed to strengthen enforcement by establishing a clear offense for unauthorised deep-sea fishing.

Previously, the law only prohibited fishing without a permit without specifying the penalties for violations. The amendment introduces a maximum fine of 1 million US dollars for anyone caught engaging in such activities without a valid license or authorisation.

The change is intended to curb frequent violations and prevent the government from losing revenue due to unlicensed deep-sea fishing.

In the Mining Act (Cap. 123), Section 100D has been amended to permit the trading of mineral concentrates within Tanzania, reversing the current prohibition. This change is designed to foster the growth of mineral refining and raw mineral industries within the country.

Additionally, Section 21F was updated to impose penalties on mineral rights holders who provide false or misleading information or fail to submit accurate mineral data.

This is intended to improve compliance with the law and ensure the accuracy of mineral data, which must now be verified by the Geological Survey of Tanzania before export.

The amendments also introduced Section 27I to formally establish the Mining Commission Mineral Laboratory, allowing it to operate on a legal basis.

Section 106 will require licensed mineral dealers and brokers to provide an integrity pledge to promote ethical standards and compliance with legal requirements.

Finally, under the Tanzania Fisheries Research Institute Act (Cap. 280), Section 24 has been repealed to resolve conflicts between the powers of the Director of Fisheries and the Board, ensuring smoother and more effective operation of the legislation.



Principal State Attorney Mark Mulwambo and his colleagues from the Attorney General's Office pictured at the High Court of Tanzania in Dar es Salaam yesterday lining themselves up for the hearing of a case filed by the Tanzania Constitutional Forum challenging the legality of the President's Office (Regional Administration and Local Governments) overseeing the local government elections slated for later this year. Photo: Correspondent Imani Nathaniel

CS Scanned with CamScanner

# Muswada wa marekebisho sheria mbalimbali watinga Bungeni

Na Joyce Kasiki, Dodoma

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, amewasilisha mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2024.

Akisoma Muswada huo jana Bungeni jijini Dodoma, Johari alisema, Muswada huo unapendekeza kufanya Marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388, Sheria ya Madini sura ya 123 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura ya 280.

Aidha, Mwanasheria Mkuu alisema, Muswada huo unapendekeza Marekebisho katika Sheria ya Usimamizi na Maendeleo ya Uvuvi katika Bahari Kuu Sura ya 388, ambapo alisema Sheria hiyo ilitungwa Mwaka 2020 baada ya kufutwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Bahari Kuu ya Mwaka 1998. Sheria hiyo haijawahi kufanyiwa marekebisho hivyo Marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hiyo ni ya kwanza.

"Spika, Ibara ya Nne ya Muswada ikisomwa pamoja na aya ya 8 ya Jedwali la Marekebisho inapendekeza Marekebisho katika kifungu cha 11 kwa madhumuni ya kuainisha Mamlaka ya Uteuzi wa Wajumbe wa Kamati ya Wataalamu ya ushauri walioainishwa katika aya za C, D, E na F, na kubainisha muda wao wa kuhudumu kama Wajumbe wa kamati, hivyo inapendekezwa kwamba wajumbe tajwa wateuliwe na Waziri mwenye dhamana ya Uvuvi na kuhudumu kwa kipindi cha miaka mitatu".

Vifungu vingine vilivyofanyiwa Marekebisho katika Sheria hiyo ni Kifungu cha 16 (1) ambacho kimependekeza kufutwa na kuandikwa upya kwa aya Ni ili kumpa Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya kuteua Maafisa wa utoaji leseni, Wakaguzi wa Uvuvi na Maafisa walioidhinishwa kutoka miongoni mwa Watumishi wa Mamlaka na kuteua Waangalizi wa Uvuvi walioko katika Mamlaka au nje ya Mamlaka.

Pia Marekebisho hayo yamegusa kifungu cha 35 cha Sheria hiyo ili kuleta masharti yanayozuia kosa la kujihusisha na shughuli zote za Uvuvi wa Bahari Kuu bila kibali halali.

Alisema Muswada huo unapendekeza kufanya Marekebisho katika Sheria ya Madini, Sura ya 123 ambayo ilitungwa Mwaka 2010, Sheria hii imeshafanyiwa marekebisho mara 13, vifungu kumi na mbili (12) vimependekezwa kufanyiwa Marekebisho katika Sheria hii, huku ikiongezwa vifungu vipya viwili (2). Katika Sheria hiyo vifungu vilivyopendekezwa kufanyiwa Marekebisho ni Vifungu vya 4, 8, 27F, 66, 73, 86A, 87, 88, 90A, 100C, 100D na 106, aidha vifungu vipya vinavyopendekezwa kuongeza ni kifungu cha 5B na 27I.

Katika hatua nyingine Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameeleza Marekebisho katika Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, Sura ya 280, ambapo amesema Muswada unapendekeza Marekebisho katika kifungu cha 21 cha Sheria hiyo ili kuongeza maneno ya nyongeza mwishoni mwa kifungu hicho yanayoweka bayana uatahwaji wa kibali cha utafiti ikiwa kutakuwa na ukiukwaji wa masharti ya utafiti.

Alisema, Muswada huo pia umependekeza kufutwa kwa kifungu cha 24 cha Sheria ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Sura ya 280, kwakua Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Uvuvi yanakinzana na Mamlaka yaliyotolewa kwa Bodi.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametumia nafasi hiyo kuwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa walyofanya katika kuandaa Muswada huo huku akiongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala, Katiba na Sheria kwa kuuchambua Muswada huo kiweledi huku akiomba Bunge kujadili na kupitisha Muswada ili kuyafanya Marekebisho hayo kuwa sehemu ya Sheria za nchi.

### Muswada mwingine

Katika hatua nyingine, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari amewasilisha bungeni muswada wa sheria wa marekebisho ya sheria mbalimbali namba mbili wa mwaka 2024 wenye sheria kuu nane.

Miongoni mwa sheria hizo ni marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54.

Mbali ya hiyo, Serikali imeondoa marekebisho kuhusu hadhi ya kumiliki ardhi kwa Watanzania wenye uraia wa nchi nyingine.

Mbunge Gekul akichangia muswada kuhusu Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 alisema: "Mimi ni mjumbe wa kamati, niunge mkono maoni ya kamati kuhusu hoja ya hadhi maalumu ambapo kamati imeshauri hata hao watu tunaotaka kuwapa hadhi maalumu ya kumiliki ardhi, kwanza wako wangapi.

"Na hizi sera ya ardhi za biashara zikiangaliwa na tukajua kama nchi tunataka kuwapa hadhi maalumu Watanzania wenzetu ambao wako nje ya nchi ni wangapi?"

Scanned with CamScanner

## Sheria Madini kufumuliwa kuruhusu biashara makinikia

Na Augusta Njoji, DODOMA

SHERIA ya Madini, Sura ya 123 imefumuliwa kupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024, na kuruhusu biashara ya makinikia ndani ya nchi ambayo awali ilikuwa imezuiliwa ili kuvutia uwekezaji katika viwanda vya madini ghafi nchini.

Akisoma maelezo ya muswada huo Bungeni jana, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, alisema sheria hiyo ilitungwa mwaka 2010 na hadi sasa imefanyiwa marekebisho mara 13.

Alisema marekebisho yanapendekeza kurekebisha jumla ya vifungu 12 na vifungu vipya viwili vinapendekezwa kuongezwa, ibara ya 21 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 100D, ili kuruhusu biashara ya makinikia ndani ya nchi. Kwa sasa sheria inazuia biashara ya makinikia ndani na nje ya nchi.

Aidha, alisema ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 106 ili kuwataka wafanyabiashara wa madini walio na leseni na mawakala au madalali walio na leseni kuapa kiapo cha uadilifu na inalenga kuhakikisha utii wa sheria.

"Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya cha 271 ili kuanzisha Maabara ya Madini ya Tume ya Madini. Lengo la marekebisho hayo ni kuirasimisha taasisi hiyo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa msingi wa sheria," alisema.

Alisema ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 66 ili kuweka adhabu kwa mtu atakayeshindwa kulipa ada ya ukaguzi kama ilivyoainishwa katika sheria.

Pamoja na hayo, alisema ibara ya 15 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 73 ili kutofautisha leseni za wafanyabiashara wa madini ya Tanzanite na wafanyabiashara wa madini ya vito vingine vya rangi.

"Lengo la marekebisho haya ni kuweka udhibiti wa madini ya Tanzanite kwa namna maalumu na kuyatangaza kwa kuzingatia uwepo wa madini hayo wa kipekee nchini Tanzania," alisema.

Alisema Muswada unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 86A ili kuweka masharti kwamba mwingizaji wa madini nchini hatatakiwa kulipa mirabaha kwa madini yanayoingizwa nchini endapo atathibitisha kuwa amelipa mirabaha katika nchi yalikotoka madini ili kuepusha ulipaji wa mirabaha zaidi ya mara moja.

"Muswada unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 87 kwa kuongeza viwango vya mirabaha inayopaswa kulipwa serikalini na wafanyabiashara wa madini ya vito yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi ambayo yamenunuliwa katika minada ya madini na maonyesho ya kimataifa ya madini ya vito," alisema.

Pia, alisema Muswada unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 27F ili kuweka adhabu kwa wamiliki wa haki za madini ambao wanatoa taarifa za uongo au zenye kupotosha au kushindwa kuwasilisha taarifa sahihi za madini.

Pia alisema ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 66 ili kuweka adhabu kwa mtu atakayeshindwa kulipa ada ya ukaguzi kama ilivyoainishwa katika sheria.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene akijadiliana jambo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari (kulia) bungeni mjini Dodoma jana. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, William Lukuvi. (Picha na Fadhili Akida).

# Ukivua bahari kuu bila kibali faini bilioni 2.7/-

Na Gloria Tesha, Dodoma

BUNGE limepitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2024 ambao pamoja na mambo mengine utadhibiti uvuvi katika bahari kuu.

Katika marekebisho hayo, makosa ya kuvua katika bahari kuu bila kibali halali yatatozwa faini kiwango cha juu dola za Marekani milioni moja (Sh bilioni 2.7).

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Johari Hamza alisema bungeni Dodoma juzi kuwa muswada huo umerekebisha sheria tatu.

Johari alizitaja sheria hizo kuwa ni Sheria ya Usimamizi wa Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388, Sheria ya Madini Sura ya 123 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Sura ya 280.

Katika muswada huo, kifungu cha 35 katika Ibara ya 6 ya Sheria ya Usimamizi wa Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 kimerekebishwa na kuweka masharti yanayoanzisha kosa la kujihusisha na shughuli zozote za uvuvi wa bahari kuu bila kibali halali.

"Kwa sasa serikali inazuia kufanya shughuli za uvuvi bila kibali lakini haijaweka sharti linaloanzisha kosa kutokana na kukiuka masharti hayo," alisema Johari.

Aliongeza: "Lengo ni kuimarisha utekelezaji kutokana na makosa hayo kufanywa mara kwa mara hivyo kusababisha serikali kupoteza mapato kutokana na kufanyika kwa shughuli za uvuvi wa bahari kuu bila vibali halali".

Kwa upande wa Sheria ya Madini Sura ya 123, kifungu kipya cha 271 kimewekwa kuanzisha Maabara ya Madini ya Tume ya Madini kuirasimisha taasisi hiyo na kuifanya itekeleze majukumu yake kisheria.

Aidha, ibara ya 15 imerekebishwa katika kifungu cha 73 ili kutofautisha leseni za wafanyabiashara wa madini ya Tanzanite na wa madini ya vito vingine vya rangi.

Serikali imesema marekebisho haya yanalenga kuweka udhibiti wa madini ya tanzanite kwa namna maalumu na kuyatangaza kwa kuzingatia uwepo wa madini hayo wa kipekee nchini Tanzania pekee.

Sheria imeondoa ulipaji wa mirabaha nchini kama muingizaji wa madini amelipa katika nchi aliyotoka kuondoa ulipaji mara mbili.

Katika hatua nyingine, sheria imeongeza kiwango cha mirabaha inayopaswa kulipwa serikalini na wafanyabiashara wa madini ya vito yanayosafirishwa kwenda nje ambayo yamenunuliwa katika minada ya madini na maonesho ya kimataifa ya madini ya vito.

"Lengo ni kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya serikali kutoka katika shughuli za madini," alisema Hamza.

Sheria imeondoa masharti kuhusu ukaguzi wa madini yanayouzwa wakati wa minada wa madini unaosimamiwa na serikali au unaotokana na maonesho ya kimataifa ya vito ikilenga kuepusha gharama za minada kwa wafanyabiashara na kuongeza ushiriki wao katika minada unaosimamiwa na serikali.

Kifungu cha 100 D kimerekebishwa kuruhusu biashara ya makinikia ndani ya nchi ili kuvutia uwekezaji wa viwanda vya madini ghafi nchini.

Kiapo cha uadilifu sasa ni takwa la kisheria kwa wafanyabiashara wa madini walio na leseni na mawakala au madalali walio na leseni.

Aidha, mtaji wa leseni ya kati ya uchimbaji madini umeanzia Dola za Marekani 5,000,000 gharama ambayo ni ukomo wa mtaji wa leseni ndogo.

Kabla ya marekebisho leseni ndogo ya uchimbaji mtaji wake ulikuwa kiasi chochote chini ya Dola za Marekani 5,000,000, leseni ya kati Dola 100,000 hadi Dola milioni 100 na leseni kubwa Dola milioni 100.

Kifungu cha 58 kimempa mamlaka waziri kutangaza baadhi ya madini kuwa ya muhimu na ya kimkakati kwa Jamhuri ya Muungano baada ya kupokea mapendekezo kutoka taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania.

Home About Us Privacy Policy Contact Us

DIRAMAKINI ARTICLES LOCAL NEWS INTER NEWS ADVERTS NI

Home › Habari

# Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 watua bungeni

**DODOMA-Mwanasheria** Mkuu wa Serikali, Mhe. Hamza Johari amewasilisha mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024].



Home About Us Privacy Policy Contact Us

DIRAMAKINI ARTICLES LOCAL NEWS INTER NEWS ADVERTS NEV

Home › Habari

# Mapendekezo ya marekebisho ya sheria nane yawasilishwa bungeni








MCHANGANYIKO

# MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI WA MWAKA 2024 WATUA BUNGENI

John Bukuku · 2 days ago
Last updated: 2024/09/02 at 5:08 PM

Share






Home Biashara Burudani Magazeti Mchanganyiko Michezo Siasa Teknolojia TV Makala

MCHANGANYIKO

# MAPENDEKEZO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NANE YAWASILISHWA BUNGENI

John Bukuku · 23 hours ago
Last updated: 2024/09/03 at 1:39 PM



**OAG Tanzania** is with **officialtcaa** and **3 others**.

1d ·

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 wawasilishwa Bungeni



**OAG Tanzania**

Reels · 3h ·




OAG UPDATES

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI MHE. HAMZA JOHARI AKIWASILISHAMUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI (NA.2) WA MWAKA 2024**

**Bungeni Jijini Dodoma**

WELEDI NA UBORA

*Kwa msaada wa huduma za Kisheria piga simu bure 0800 11 0188*

oagtanzania OAG TV www.oag.go.tz @oag_tz

# TUPO KARIBU YAKO!

## Tufuatilie kupitia

oagtanzania

info@oag.go.tz

www.oag.go.tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania

**KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188**

Weledi na Ubora